

MAKALA-IDARA YA UJENZI 2017.

Idara ya Ujenzi katika Manispaa ya Kinondoni pamoja na Mambo mengine inajukumu la kusimamia utoaji wa vibali vya ujenzi kwa kushirikiana na Idara za Mipangomiji na mazingira, Afya na zimamoto ambazo huchunguza maombi ya ramani za majengo kama zinakidhi kupata kibali cha ujenzi kufuatana na sheria inayosimamia ujenzi mjini sura Na.288 na kanuni yake ya mwaka 2008.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Idara hii ilipokea jumla ya maombi 2022 ya vibali vya ujenzi ambapo kati ya vibali hivyo, vibali vikubwa vilikuwa 828, na vibali vidogo vilikuwa 366. Aidha kati ya maombi 828 ya vibali vikubwa vya ujenzi idara ilifanikiwa kutoa jumla ya vibali 716 huku maombi 120 yakikosa vibali kutokana na kutokidhi vigezo ambapo yanaendelea kuchunguzwa kwa ushirikiano mkubwa na wa karibu na idara nyingine kuhakikisha yanakidhi vigezo na kupewa vibali.

Miongoni mwa changamoto katika eneo hili ni wananchi wengi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vibali vya ujenzi na umuhimu wake, uhaba wa vyumba vya kufanyia kazi na kuhifadhi nyaraka, upungufu wa watumishi, ukosefu wa usafiri na changamoto ya utaratibu mrefu wa kupata kibali kwa maeneo yasiyopimwa. Hata hivyo Mkuu wa Idara hii Bwana Justin Lukaza amejizatiti kuendelea kutoa elimu na kuongeza vitendea kazi ili kuweza kukabiliana nazo na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Katika suala zima la usimamizi wa miradi ya maendeleo idara ya ujenzi inajukumu la kusimamia miradi yote ya ujenzi wa majengo ya Idara na vitengo Mbalimbali vya Manispaa ya Kinondoni ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 katika Idara ya Elimu ya Sekondari imeweza kusimamia ujenzi wa vyumba 12 vya madarasa Mivumoni sekondari, ujenzi wa madarasa 2 Kigogo Sekondari, ujenzi wa madarasa 4 Salma Kikwete Sekondari, ujenzi wa Madarasa 3 njechele Sekondari, Madarasa 3 Mabwe Sekondari, madarasa 2 Makongo juu sekondari, madarasa 4 Bunju A sekondari, madarasa 4 Mbezi juu sekondari, madarasa 6 Mzimuni sekondari, madarasa 4 Mbweni Teta sekondari, ujenzi wa nyumba ya mwalimu Mabwe sekondari, ujenzi wa matundu 10 ya vyoo Maendeleo Sekondari, matundu 12 Kambangwa Sekondari, matundu 12 Kondo sekondari, matundu 12 Mzimuni sekondari, matundu 12 Oysterbay sekondari, matundu 10 Mbweni Teta sekondari, na ujenzi wa nyumba za walimu, uzio, na bwalo Tumaini Girls Sekondari.

Katika Idara ya Elimu ya Msingi Miradi ya Ujenzi iliyosimamiwa ni Pamoja na ukamilishaji wa chumba cha darasa Hekima shule ya msingi, ukarabati wa vyumba 3 vya madarasa Mwananyamala Kisiwani, vyumba 3 vya madarasa Ukwamani shule msingi, kukamilisha madarasa 2 Mbopo shule ya msingi, ujenzi wa madarasa 2 Bunju shule ya msingi, madarasa 5 Mapinduzi shule ya msingi, ujenzi wa matundu 12 ya vyoo katika shule za msingi Boko,,Magomeni, Muhaltan, Hekima, Mirambo, Kawe B, Mbezi Beach, Tandale Magharibi, Mzimuni, Bongoyo, Ujenzi wa uzio Gilman Lutihinda, ukarabati wa madarasa 7 shule ya msingi Msasani B, vyumba 2 kituo cha walimu Kunduchi, madarasa 3 Mapambano shule ya msingi, darasa 1 Shule msingi Mwananyamala, na madarasa 2 shule ya msingi Msasani.

Katika Idara ya Afya Miradi ya Ujenzi iliyosimamiwa ni pamoja na ujezi wa wodi ya wazazi katika Hospitali ya Mabwepande, ujenzi wa nyumba 2 za watumishi hospitali ya Mabwepande, ujenzi wa jengo la RCH Hospitali ya Mabwepande, Ukarabati wa Kituo cha Afya Kata ya Kigogo na ujenzi wa

Idara nyingine yenye miradi ya ujenzi ni Utawala na Utumishi yenye mradi wa umaliziaji wa ujenzi wa ofisi ya Kata Kigogo, Idara ya Kilimo na Mifugo yenye mradi wa ukarabati wa Ofisi ya Kilimo na Mifugo, ugawaji wa vyumba vya ofisi kwa kutumia kontena Malolo, ujenzi wa Karakana ya kugesha magari kituo cha kilimo Malolo, ujenzi wa ofisi ya Ardhi Makao makuu ya Manispaa Magomeni, Ujenzi wa Soko la Msufini, ukarabati

wa soko la samaki Kunduchi ,kukamilisha ujenzi wa machinjio ya kuku Kawe na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua katika kata na Mitaa mbalimbali.

Mwisho, Kwa kuzingatia Umuhimu wa Miradi ya ujenzi ndani ya Manispaa ya Kinondoni, Idara ya ujenzi imejiwekea dhamira ya kusimamia kwa karibu miradi yote Kwa kushirikiana na idara husika ili iweze kutekelezwa kwa viwango bora na kuzingatia thamani ya fedha yaani Value of Money.



Picha ya ujenzi wa mfereji wa maji ya mvua kuelekea baharini.



Picha ya jengo la Hospital ya Wilaya, iliyoko Mabwepande.

